TANGAZO LA SERIKALI NA. 42 la tarehe 24/1/2025

SHERIA YA UNUNUZI WA UMMA,
(SURA YA 410)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya Kifungu cha 129)*

## KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UNUNUZI WA UMMA ZA MWAKA 2025

Jina

TS. Na. 518 la 2024

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Ununuzi wa Umma, za Mwaka 2024 ambazo katika Kanuni hizi zinarejewa kama "Kanuni kuu".

Marekebisho ya Kanuni ya 4

**2**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 4(1) kwa kuongeza maneno "kwa mujibu wa Sheria za Tanzania na mikataba ya kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania inayosimamia mazingira" mara baada ya neno "ugavi".

Marekebisho ya Kanuni ya 5

**3**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 5-

(a) kwa kuongeza mara baada ya Kanuni ndogo ya (6) Kanuni Ndogo ifuatayo:

> "(7) Kwa madhumuni ya Kanuni Ndogo ya (6) na kwa kuzingatia Kanuni ya 167, kampuni au wakala unaoitegemea taasisi nunuzi utachukuliwa kuwa sehemu ya taasisi nunuzi husika."; na

(b) kwa kubadili mpangilio wa Kanuni Ndogo ya (7) kuwa Kanuni Ndogo ya (8).

Marekebisho ya Kanuni ya 7

**4**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 7(6)(e) kwa kufuta maneno "zisizo za ushauri elekezi".

Marekebisho ya Kanuni ya 23

**5**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 23(8) kwa kuongeza maneno "ambazo zitapaswa kuthibitishwa au kuhakikiwa na benki za ndani au kampuni za bima za ndani zinazotambulika" mara baada ya neno "yoyote" lililopo mwishoni.

Marekebisho ya Kanuni ya 40

**6**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 40-

(a) kwa kufuta maneno "iliyopewa tuzo ya mkataba wa ununuzi" katika Kanuni Ndogo ya (1);
(b) kwa kufuta Kanuni Ndogo ya (6); na
(c) kwa kubadili mpangilio wa Kanuni Ndogo ya (7) kuwa Kanuni Ndogo ya (6).

Marekebisho ya Kanuni ya 41

**7**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 41-

(a) kwa kufuta Kanuni Ndogo ya (1) na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"(1) Wazabuni wa kigeni wanaweza, kwa lengo la kupata upendeleo katika zabuni za ununuzi wa umma, kuingia katika ubia na wazabuni wa ndani.";

(b) kwa kufuta Kanuni Ndogo ya (2);
(c) katika Kanuni Ndogo ya (3), kwa kufuta rejea ya "Kanuni Ndogo ya (2)" na badala yake kuweka rejea ya "Kanuni Ndogo ya (1)";
(d) katika Kanuni Ndogo ya (6), kwa kufuta rejea ya "Kanuni Ndogo ya (5)" na badala yake kuweka rejea ya "Kanuni Ndogo ya (4)"; na
(e) kwa kubadili mpangilio wa Kanuni Ndogo za (3), (4), (5) na (6) kuwa Kanuni Ndogo za (2), (3), (4) na (5) mtawalia.

Marekebisho ya Kanuni ya 42

**8**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 42(4) kwa kufuta rejea ya "Kanuni Ndogo ya (1)" na badala yake kuweka rejea ya "Kanuni Ndogo za (1) na (2)".

Marekebisho ya Kanuni ya 48

**9**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 48(7) kwa kufuta neno "hamsini" na badala yake kuweka maneno "ishirini na tano".

Marekebisho ya Kanuni ya 49

**10**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 49(1) kwa kuongeza maneno "katika maeneo yatakayobainishwa kwenye nyaraka ya zabuni na taasisi nunuzi" mara baada ya neno "uwezo".

Marekebisho ya Kanuni ya 123

**11**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 123(3)-

(a) kwa kufuta aya (a); na

(b) kwa kubadili mpangilio wa aya (b) na (c) kuwa aya (a) na (b) mtawalia.

Marekebisho ya Kanuni ya 134

**12**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 134-

(a) katika Kanuni Ndogo ya (1), kwa kufuta maneno "afisa masuuli atapaswa" yaliyopo katika maneno ya ufunguzi na badala yake kuweka maneno "Bohari ya Dawa itapaswa";

(b) katika Kanuni Ndogo ya (5), kwa kufuta maneno "Afisa masuuli atatoa" na badala yake kuweka maneno "Bohari ya Dawa itatoa"; na

(c) katika Kanuni Ndogo ya (7), kwa kufuta maneno "Taasisi nunuzi zitatumia" na badala yake kuweka maneno "Bohari ya Dawa itatumia".

Marekebisho ya Kanuni ya 162

**13**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 162(1) kwa kufuta maneno "sifa za ubora na vigezo vya kiufundi vya zabuni" na badala yake kuweka maneno "masuala ya ubora na ya kiufundi ya zabuni husika".

Marekebisho ya Kanuni ya 171

**14**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 171(2) kwa kufuta tarakimu "322" na badala yake kuweka tarakimu "313A".

Marekebisho ya Kanuni ya 226

**15**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 226 kwa kufuta maneno "zingine zozote".

Marekebisho ya Kanuni ya 230

**16**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 230(5) kwa kufuta maneno "Kundi A au Kundi B" na badala yake kuweka maneno "Kundi A, Kundi B au Kundi C".

Marekebisho ya Kanuni ya 233

**17**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 233 kwa kuongeza mara baada ya Kanuni Ndogo ya (9) Kanuni Ndogo ifuatayo:

"(10) Endapo muafaka hautafikiwa ndani ya muda wa majadiliano ulioongezwa, majadiliano yatachukuliwa kuwa yameshindikana na timu ya majadiliano itapendekeza kukataliwa kwa mzabuni, na endapo itaonekana inafaa, kupendekeza kumwalika mzabuni mshindi anayefuata kwa ajili ya majadiliano.".

Kuongezwa Kanuni ya 313A

**18**. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya Kanuni ya 313 Kanuni mpya ifuatayo:

"Kamati ya ukaguzi na mapokezi

**313A**.-(1) Afisa Masuuli atateua kwa kila zabuni kamati ya ukaguzi na mapokezi ya bidhaa, kazi za ujenzi au huduma ambayo itaundwa na wajumbe watatu mmoja kutoka katika Idara tumizi na wengine wenye utaalamu wa masuala ya ununuzi au eneo la mradi.

(2) Katika mazingira ya kipekee, Afisa Masuuli anaweza kuunda kamati ya ukaguzi na mapokezi yenye wajumbe zaidi ya watatu kulingana na thamani na ugumu wa ununuzi endapo kuna sababu za msingi za ongezeko hilo na idadi witiri ya wajumbe itazingatiwa.

(3) Kamati ya ukaguzi na mapokezi itapaswa-

(a) kukagua na kupokea bidhaa, kazi za ujenzi au huduma katika eneo litakaloainishwa kwenye mkataba au eneo lingine lolote baada ya kupata idhini ya taasisi nunuzi;
(b) kukagua bidhaa, kazi za ujenzi au huduma kwa lengo la kubaini endapo zimewasilishwa au kukamilika kwa wakati, ziko sahihi, kamili na zenye ubora kwa mujibu wa mkataba;
(c) kukataa bidhaa, kazi za ujenzi au huduma ambazo hazijakamilika au hazijakidhi masharti ya mkataba;
(d) kukagua nyaraka zote muhimu; na
(e) kuandaa taarifa ya ukaguzi na kuiwasilisha kwa Afisa Masuuli kwa hatua stahiki.

(4) Pale ambapo mjumbe wa kamati ya ukaguzi na mapokezi amekataa kupokea bidhaa, kazi za ujenzi au huduma zilizowasilishwa kwa kuandika maoni ya kutokukubaliana, kamati itawasilisha taarifa hiyo kwa Afisa Masuuli kwa hatua stahiki.”.

Kufutwa kwa Kanuni ya 322

**19**. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta Kanuni ya 322.

Marekebisho ya Kanuni ya 324

**20**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 324 kwa kuongeza mara baada ya Kanuni Ndogo ya (3) Kanuni Ndogo zifuatazo:

"(4) Endapo muuzaji atashindwa kuondoa bidhaa ndani ya muda ulioainishwa chini ya Kanuni Ndogo ya (3), taasisi nunuzi inaweza, iwapo itaona inafaa au kwa sababu za msingi zilizotolewa na mzabuni, kuongeza muda usiozidi siku kumi na nne.

(5) Endapo mzabuni atashindwa kuondoa bidhaa ndani ya muda ulioainishwa katika Kanuni Ndogo za (3) na (4), bidhaa hizo zitachukuliwa kuwa zimetelekezwa na zitashughulikiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Fedha za Umma na Kanuni zake.".

Sura ya 348

Marekebisho ya Kanuni ya 329

**21**. Kanuni kuu zinarekebishwa katika Kanuni ya 329(5) kwa kufuta maneno "kurekebisha dosari au kukamilisha kazi za ujenzi" na badala yake kuweka maneno "au kurekebisha dosari".

Dodoma,
31 Desemba, 2024

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU,
*Waziri wa Fedha*